

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 42 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** AGOSTI 2024

TSC KUSHIRIKI MAONESHO YA NANENANE JIJINI DODOMA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimsikiliza mteja aliyetembelea banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima Nanenane ya mwaka 2023 yaliyofanyika mkoani Mbeya.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

RAIS SAMIA ANAENDELEA KUSIMAMIA MASLAHI YA WALIMU, WALIMU TUHAKIKISHE TUNATIMIZA WAJIBU WETU

Ni wazi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuonesha nia ya kuhakikisha anamaliza kero na changamoto mbalimbali za walimu. Malalamiko mengi ya walimu yalikuwa yanahusu kucheleweshwa kupandishwa vyeo, kucheleweshwa kubadilishiwa cheo baada ya kukidhi vigezo, madai ya fedha za likizo na uhamisho pamoja na malimbikizo ya mishahara.

Rais Samia ameendelea kushughulikia changamoto hizo kwa kiasi kikubwa; Walimu wameendelea kulipwa fedha zao, wameendelea kubadilishiwa vyeo vyao lakini kubwa zaidi ni walimu kupandishwa vyeo na wengine kwa mserereko ili kupata cheo/daraja linalostahili kwa mujibu wa taratibu.

Dhamira hii ya Mhe. Rais inapaswa kuungwa mkono na kila mwalimu kwa kuhakikisha

tunatimiza wajibu wetu kikamilifu. Wajibu mkuu wa mwalimu ni kufundisha. Walimu huandaa masomo, kusimamia kazi za wanafunzi darasani na kukutana na wazazi. Aidha, zaidi ya kutekeleza mipango ya masomo (kufundisha), mwalimu pia hufanya majukumu ya ulezi na ushauri kwa mwanafunzi.

Kama Mtumishi wa Umma, Mwalimu ana wajibu wa kutoa huduma kwa wananchi mbalimbali katika maeneo na ngazi tofauti tofauti, kuheshimu sheria, kuzingatia maelekezo na maagizo halali na kutekeleza kazi zote za Mwajiri wake kwa kuzingatia utaratibu na kwa mujibu wa mgawanyo wa kazi/majukumu.

Ni wajibu wa kila mwalimu kuhakikisha anawajibika ipasavyo katika sehemu yake ili elimu yetu izidi kuwa bora na Taifa letu lizidi kuwa na maendeleo.

KATUNI

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu


Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TSC KUSHIRIKI MAONESHU YA NANENANE JIJINI DODOMA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa Taasisi mbalimbali za Serikali zitakazoshiriki Maonesho ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi (Nane Nane) Kitaifa yatakayofanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 1 - 8 Agosti, 2024.

Katika Maonesho hayo, TSC inakusudia kutoa huduma kwa walimu na wateja wengine watakaofika kwenye banda la Tume hiyo.

Maonesho ya Nanenane kwa mwaka 2024 yana Kauli Mbiu isemayo "Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi".

Akizungumza na waandishi wa Habari hivi karibuni jijini Dodoma, Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb), alisema maonesho hayo yataendelea kuwa ya



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimsikiliza mteja aliyetembelea banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima Nanenane ya mwaka 2023 yaliyofanyika mkoani Mbeya.

Kimataifa ambapo tayari baadhi ya nchi jirani zimethibitisha kushiriki.

Aliongeza kuwa kampuni mbalimbali zinazonunua na kuuza bidhaa za kilimo zitashiriki katika

kanda saba (7) ambazo ni Kanda ya Nyanda za Juu Kusini jijini Mbeya kwenye uwanja wa John Mwakangale; Kanda ya Mashariki mjini Morogoro kwenye viwanja vya Mwl. Julius Kambarage Nyerere; Kanda ya Kusini mjini Lindi kwenye viwanja vya Ngongo; Kanda ya Ziwa Magharibi jijini Mwanza katika viwanja vya Nyamhongolo; Kanda ya Ziwa Mashariki mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi; Kanda ya Kaskazini jijini Arusha kwenye viwanja vya Them; na Kanda ya Magharibi mjini Tabora kwenye viwanja vya Fatma Mwasa.

Tume ya Utumishi wa Walimu itakuwa katika eneo moja litakalojumuisha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zake zikiwemo Chuo cha Serikali za Mitaa, TARURA, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Shirika la Elimu Kibaha na Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (Dart).



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa na wanafunzi waliotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima Nanenane ya mwaka 2023 yaliyofanyika mkoani Mbeya.

KATIBU TSC ATEMBELEA WATAALAMU WA KUUNGANISHA MFUMO WA TSCMIS NA MIFUMO MINGINE

Na Mwandishi wetu – Morogoro.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 04 Julai, 2024 alitembelea Wataalam wanaofanya kazi ya kuunganisha Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (Teachers' Service Commission Management Information System -TSCMIS) na Mifumo mingine ya Serikali ili iweze kubadilishana taarifa na kurahisisha utoaji huduma za kiutumishi kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara.

Kazi hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Hazina, mjini Morogoro.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na Wataalam wanaofanya kazi ya kuunganisha Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (Teachers' Service Commission Management Information System -TSCMIS) na Mifumo mingine ya Serikali tarehe 04 Julai, 2024 mjini Morogoro.

KATIBU TSC ATEMBELEA WATAALAMU WA KUUNGANISHA MFUMO WA TSCMIS NA MIFUMO MINGINE



Wataalamu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na nje ya TSC wakiendelea na kazi ya kuunganisha mfumo wa TSCMIS na mifumo mingine ya Serikali ili iweze kubadilishana taarifa.

KATIBU TSC AWAONGOZA WAOMBOLEZAJI KUAGA MWILI WA JULIUS NDUMBARO

**Na Mwandishi Wetu –
Dodoma.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama ameongoza watumishi wa TSC na wananchi wengine waliojitokeza kuaga mwili wa aliyekuwa Mtumishi wa Tume hiyo, marehemu Julius Mathew Ndumbaro aliyefariki tarehe 27 Julai, 2024.

Marehemu Ndumbaro aliyekuwa Msaidizi wa Ofisi TSC Makao Makuu Dodoma alifariki wakati akiendelea na matibabu



Mwili wa marehemu Julius Mathew Ndumbaro ukiwa unapokelewa na waombolezaji tarehe 30 Julai, 2024 mara baada ya kuwasili nyumbani kwake, Mailimbili jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akitoa heshima zake za mwisho kwa marehemu Julius Mathew Ndumbaro mara baada ya Misa iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Kiwanja cha Ndege jijini Dodoma kabla kusafirishwa kuelekea mkoani Ruvuma kwa mazishi.

katika Hospitali ya Kanda ya Benjamini Mkapa jijini Dodoma.

Akisoma wasifu wa Marehemu kwa niaba ya Katibu wa TSC, Afisa Utumishi Mkuu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Francis Gwankisa, alisema kuwa marehemu alikuwa mchapakazi na rafiki ya kila mtumishi.

"Kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tumepoteza rafiki, ndugu na mchapakazi, mchango wake tutaendelea kuukumba, "alisisitiza.

Alisema kuwa Tume ikiongozwa na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu Prof. Masoud Hadi Muruke, Makamishna, Katibu wake na Watumishi wote wako pamoja na familia na Mungu awape nguvu katika kipindi kigumu cha kuondokewa na Mpendwa wao.

Marehemu Ndumbaro anatarajiwa kuzikwa tarehe 31 Julai, 2024 Bombambili Songea mkoani Ruvuma.

KATIBU TSC AWAONGOZA WAOMBOLEZAJI
KUAGA MWILI WA JULIUS NDUMBARO

Mwili wa marehemu Julius Mathew Ndumbaro ukiwa unapokelewa na waombolezaji tarehe 30 Julai, 2024 mara baada ya kuwasili nyumbani kwake, Mailimbili jijini Dodoma.



Mwili wa marehemu Julius Mathew Ndumbaro ukiwa unatolewa nyumbani jijini Dodoma kwa ajili ya kuelekea Kanisani tarehe 30 Julai, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) akizwa na baadhi ya viongozi TSC wakati akisubiri kutoa heshima za mwisho kwa marehemu Julius Mathew Ndumbaro.



Mwili wa marehemu Julius Mathew Ndumbaro ukitolewa Kanisani tarehe 30 Julai, 2024 mara baada ya Misa ya Kuuaga katika Kanisa la Kiwanja cha Ndege jijini Dodoma.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Ninatoa pole kwa familia, Katibu, Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu TSC kutokana na kifo cha Mtumishi wa Tume **Bw. Julius Ndumbaro** kilichotokea tarehe 27 Julai, 2024 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

**BWANA ALITOA NA BWANA
AMETWAA JINA LA BWANA
LIHIMIDIWE**

**Prof. Masoud Hadi Muruke
Mwenyekiti TSC**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

MWENYEKITI WA TSC AWAONGOZA WATUMISHI WA TUME KUTOA HESHIMA ZA MWISHO KWA MAREHEMU MAIMUNA

**Na Mwandishi wetu –
Dar es Salaam.**

Mwenye kiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Masoud Muruke ameongoza mamia ya watu katika mazishi ya Mtumishi wa TSC, Bi. Maaaimuna Mustapha Kuhenga, tarehe 30 Julai, 2024.

Mazishi hayo yalihudhuriwa pia na Watumishi wa Tume kutoka Makao Makuu Dodoma na walioko jijini Dar es salaam.

Akitoa salamu za Tume, Prof. Muruke alisema kuwa Marehemu Maimuna ambaye alikuwa mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu Dodoma kwa nafasi ya Afisa Kumbukumbu Daraja II alifariki jijini Dar es Salaam alikuwa mmoja wa watumishi waliokuwa wanafanya kazi kwa bidii, weledi na maoyo wa kujituma, pia alikuwa rafiki wa kila mtu.

“Kwa upande wa Tume ya



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akitoa pole kwa mume wa aliyekuwwa Mtumishi wa TSC, Marehemu bi. Maimuna Kuhenga wakati wa mazishi ya mtumishi huyo yaliyofanyika tarehe 30 Julai, 2023 jijini Dar es Salaam.

Utumishi wa Walimu (TSC) tumepoteza rafiki, ndugu na mchapakazi, mchango wake tutaendelea kuukumba,” alisisitiza.

Alisema kuwa viongozi wa Tume na Watumishi wote wako pamoja

na familia na Mungu awape nguvu katika kipindi kigumu cha kuondokewa na Mpendwa wao.

Marehemu Maimuna alizikwa tarehe 30 Julai, 2024 , jijini Dar es Salaam.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akiwa na watumishi wengine waliohudhuria mazishi ya aliyekuwwa mtumishi wa TSC Marehemu bi. Maimuna Kuhenga yaliyofanyika tarehe 30 Julai, 2023 jijini Dar es Salaam.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke ametoa pole kwa Familia, Katibu, Makamishna na Watumishi wote wa TSC kutokana na kifo cha Mtumishi wa Tume, **Bi. Maimuna Kuhenga** kilichotokea usiku wa kuamkia leo tarehe 29 Julai 2024.

*Marehemu Maimuna alikuwa msaidizi
wa Kumbukumbu TSC Makao Makuu.*

'Innalilah wainnailah rajiun.'



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



Makuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Lameck Mbeya (kushoto) akikagua nalaka za vitabu vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja vya TSC kutoka kwa Mzabuni aliyeandaa vitabu hivyo, Bi. Jemima Jackson.



Makuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Lameck Mbeya (kushoto) akikagua nalaka za vitabu vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja vya TSC kutoka kwa Mzabuni aliyeandaa vitabu hivyo, Bi. Jemima Jackson.




Makuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Lameck Mbeya (kushoto) akipokea nalaka za vitabu vya Mkataba wa Huduma kwa Mteja vya TSC kutoka kwa Mzabuni aliyeandaa vitabu hivyo, Bi. Jemima Jackson.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Wajibu wa Mwalimu kwa mtoto, mwajiri, kazi, jamii na Taifa



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC MBIONI KUKAMILISHA UFUNGAMANISHI WA TSCMIS NA MIFUMO MINGINE

Na Mwandishi Wetu – TSC, Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iko katika hatua za mwisho za kukamilisha kazi ya kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine ili iweze kubadilishana taarifa.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 23 Julai, 2024 mjini Morogoro na Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bi. Kainda Ndasa wakati wa mahojiano maalum na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC.

Alisema Mfumo huo utakuwa na Moduli sita ikiwa ni pamoja na inayoshughulikia mashauri ya kinidhamu, rufaa, usajili wa walimu, mirathi na pesheni, malalamiko (complaints) na inayoratibu wageni wanaotembelea Ofisi za TSC.

Bi. Kainda aliongeza kuwa TSCMIS imeweza kuunganishwa na mifumo mbalimbali ikiwemo Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi (e-Watumishi), Mfumo wa Malipo ya Pesheni (TPPS) Mfumo wa Taarifa za Shule (SIS) ambao utawezesha kujua mahudhurio, vipindi vinavyofundishwa na shule zenyewe.

Alisema kuwa kwa upande wa moduli ya wageni, TSC itaweza kupata taarifa za wageni waliotembelea Tume na hoja au maswali waliyouliza.

Bi. Kainda alisema kuwa katika kushughulikia masuala ya nidhamu kwa walimu, mfumo utakuwa na hatua tatu ukianzia ngazi ya Shule ambapo Mkuu wa Shule atakuwa na uwezo wa kupitia suala la nidhamu na kuchukua hatua, kisha katika ngazi ya wilaya mwalimu anaweza kufunguliwa shauri la kinidhamu na pia yeye anayo nafasi ya kukata

rufaa kupitia kwenye Mfumo huo.

Alisema kwa upande wa Ofisi za TSC Makao Makuu zitakuwa na uwezo wa kupokea rufaa na kushughulikia na pia TSC makao makuu itaweza kupata taarifa (report) kutoka Ofisi za Wilaya.

Bi. Kainda alisema kuwa hadi sasa kazi kubwa imeshafanyika wanachoendelea nacho ni majaribio ya mfumo ili kuona utendaji kazi wake.

Naye Mwenyekiti wa Timu ya Wataalamu hao ambaye ni Afisa TEHAMA Mwandumizi kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Bw. Shaban Zungiza alisema katika ufunganishaji wa mfumo huo na mifumo mingine wameshughulikia maboresho na

kuandaa dirisha maalumu (mobile App) ambalo litasaidia mwalimu kupata taarifa hata kwa kutumia simu zao.

Zoezi hilo ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha ifikapo Desemba mwaka 2024 mifumo ndani ya Serikali iwe inasomana.

Wataalamu hao wanatoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).



Wataalamu wakiendelea na zoezi la kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine ya Serikali.



Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Kainda Ndasa (kushoto) akiwa na Wataalamu wakiendelea na zoezi la kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine.

TSC MBIONI KUKAMILISHA UFUNGAMANISHI WATSCMIS NA MIFUMO MINGINE



Wataalamu wakiendelea na zoezi la kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine ya Serikali.



Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Kainga Ndasu (kushoto) akiwa na Wataalamu wakiendelea na zoezi la kufungamanisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Julai
25

SIKU YA MASHUJAA



Tunaungana na Watanzania wote kuenzi na kukumbuka
mchango wa Mashujaa wetu waliopigana vita kwa ajili ya
uhai wa Taifa la Tanzania



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

Kamati ya Ukaguzi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya kikao chake tarehe 1 Julai, 2024 kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayojitokeza katika Ukaguzi wa Ndani unaofanyika TSC.

Kikao hicho cha kawaida kilifanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za TSC Makao Makuu zilizopo Mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma.





Mkurugenzi wa Huduma za Sheria Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akisaini daftari la wageni alipotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria tarehe 03 Julai, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma. Pembuni yake ni Afisa Sheria wa TSC, Wakili Selina Magoiga.




Mkurugenzi wa Huduma za Sheria Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo (kulia) akisikiliza maelezo kutoka kwa Afisa Sheria wa TSC, Wakili Selina Magoiga wakati alipotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria tarehe 03 Julai, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu